TAARIFA YA MAELEZO YA CHANJO

Chanjo ya Hib

Unachohitaji Kujua

(*Homa ya Mafua ya Haemofilia ya Aina* b)

Many Vaccine information Statements are available in Spanish and other languages. See www.immunize.org/vis
Hojas de información sobre vacunas están disponibles en español y en muchos otros idiomas. Visite www.immunize.org/vis

1 Kwa nini nipokee chanjo?

Ugonjwa wa haemophilus influenzae aina ya b (Hib) ni ugonjwa hatari unaosababishwa na bakteria. Huwa unaathiri watoto chini ya umri wa miaka 5. Pia unaweza kuathiri watu wazima wenye hali fulani za kimatibabu.

Mtoto wako anaweza kupata ugonjwa wa Hib kwa kawa karibu na watoto wengine au watu wazima ambao huenda wakawa na bakteria hiyo na wasijue. Viini hivi husambaa kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine. Ikiwa viini hivi vitasalia katika pua na koo ya mtoto, huenda mtoto asiwe mgonjwa. Lakini wakati mwingine viini hivi husambaa kwenye mapafu au kwenye damu, na kisha Hib inaweza kusababisha matatizo hatari. Jambo hili linaitwa ugonjwa vamizi wa Hib.

Kabla ya chanjo ya Hib, ugonjwa wa Hib ulikuwa sababu inayoongoza ya homa ya uto wa mgongo ya bakteria kati ya watoto chini ya umri wa miaka 5 nchini Marekani. Homa ya uti wa mgongo ni maradhi ya mpangilio wa ubongo na uti wa mgongo. Ugonjwa huu unaweza kusababisha uharibifu wa ubongo na uziwi. Ugonwja wa Hib unaweza pia kusababisha:

- nimonia
- uvimbe mkali katika koo, na kusababisha ugumu wa kupumua
- maradhi ya damu, viungo, mifupa, na ufunikaji wa moyo
- kifo

Kabla ya chanjo ya Hib, takriban watoto 20,000 nchini Marekani chini ya umri wa miaka 5 waliugua ugonjwa wa Hib kila mwaka, na takriban 3% - 6% ya watoto hao walikufa.

Chanjo ya Hib inaweza kuzuia ugonjwa wa Hib. Tangu matumizi ya chanjo ya Hib kuanza, idadi ya visa vya ugonjwa vamizi wa Hib vimepungua kwa zaidi ya 99%. Watoto wengi zaidi wataugua ugonjwa wa Hib tukiwacha kupeana chanjo.

2 Chanjo ya Hib

Chapa tofauti kadhaa za chanjo ya Hib zinapatikana. Mtoto wako atapokea aidha dozi 3 au 4, kulingana na aina ya chanjo inayotumiwa.

Dozi za chanjo ya Hib hupendekezwa kwa umri huu:

- Dozi ya Kwanza: umri wa miezi 2
- Dozi ya Pili: umri wa miezi 4
- Dozi ya Tatu: umri wa miezi 6 (ikiwa inahitajika, kulingana na chapa ya chanjo)
- Dozi ya Mwisho/Nyongeza: umri wa miezi 12 -15

Chanjo ya Hib inaweza kupeanwa kwa usalama wakati wowote kama chanjo zingine.

Chanjo ya Hib inaweza kupeanwa kama sehemu ya chanjo mchanganyiko. Chanjo mchanganyiko hutengenezwa wakati aina mbili au zaidi za chanjo zinachanganywa pamoja kwenye sindano moja, ili chanjo moja iweze kulinda dhidi ya zaidi ya ugonjwa mmoja.

Watoto wenye umri zaidi ya miaka 5 na watu wazima kwa kawaida huwa hawahitaji chanjo ya Hib. Lakini inaweza kupendekezwa kwa watoto wakubwa au watu wazima wenye asplenia au ugonjwa wa selimundu, kabla ya upasuaji wa kuondoa wengu, au baada ya upandikizaji wa uboho. Pia inaweza kupendekezwa kwa watu wenye umri wa miaka 5 hadi 18 walio na UKIMWI. Muulize daktari wako maelezo.

Daktari wako au mtu anayekupatia chanjo hii anaweza kukupatia maelezo zaidi.

3 Baadhi ya watu hawafai kupokea chanjo hii

Chanjo ya Hib haifai kupewa watoto wachanga chini ya umri wa wiki 6.

Mtu yoyote ambaye ashawahi kuwa na mzio wa kuhatarisha maisha baada ya kupokea dozi ya chanjo ya Hib, AU ana mzio mkali dhidi ya sehemu ya chanjo hii, hafai kupokea chanjo ya Hib. *Mwambie mtu anayetoa chanjo kuhusa mizio yoyote mikali*.

Watu wagonjwa kidogo wanaweza kupokea chanjo ya Hib. Watu wagonjwa wastani au mahututi wanafaa kusubiri hadi wapone. Zungumza na mtoa huduma wako wa afya ili mtu anayepokea chanjo hahisi vizuri siku ya chanjo.

U.S. Department of Health and Human Services
Centers for Disease Control and Prevention

4 Hatari za mzio wa chanjo

Ukitumia dawa zozote, hata chanjo, huwa kuna uwezekano wa madhara. Madhara haya huwa sio hatari na hupotea yenyewe. Mizio hatari pia inawezekana lakini ni nadra.

Watu wengi wanaopata chanjo ya Hib huwa hawapati matatizo yoyote nayo.

Matatizo Yasiyo Hatari baada ya kupokea chanjo ya Hib:

- wekundu, joto, au uvimbe kwenye sehemu iliyodungwa sindano
- homa

Matatizo haya sio ya kawaida. Ikiwa yatatokea, huanza mara tu baaada ya kupokea sindano na huchukua siku 2 au 3.

Matatizo yanayoweza kutokea baada ya chanjo yoyote:

Dawa zozote zinaweza kusababisha mzio mkali. Mizio kama hii kutoka kwa chanjo huwa nadra sana, inakadiriwa chini ya dozi 1 kati ya dozi milioni moja, na inaweza kutokea ndani ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

Kama tu dawa zozote, kuna nafasi ndogo sana ya chanjo kusababisha majeraha makali au kifo.

Watoto wakubwa, vijana, na watu wazima wanaweza pia kupata matatizo haya baada ya chanjo yoyote:

- Wakati mwingine watu huzimia baada ya utaratibu wa matibabu, ikiwa ni pamoja na chanjo. Kuketi au kulala chini kwa takriban dakika 15 kunaweza kusaidia kuzuia kuzirai, na majeraha yanayosababishwa na kuanguka. Mwambie daktari wako ikiwa unahisi kizunguzungu, au kubadilika kwa namna unavyoona au kelele katika masikio.
- Watu wengine hupata maumivu makali mabegani na huwa na ugumu wa kusongeza mkono mahali ambapo sindano ilidungwa. Jambo hili hufanyika mara chache sana.

Usalama wa chanjo hufuatiliwa wakati wote. Kwa maelezo zaidi, tembelea: **www.cdc.gov/vaccinesafety/**

5 Na kukiwa na mzio hatari?

Ninafaa kutafuta nini?

- Tafuta kitu chochote kinachokutia wasiwasi, kama vile dalili za mzio mkali, homa kali sana, au tabia isiyo ya kawaida.

Dalili za mzio mkali zinaweza kujumuisha mabaka ngozini, uvimbe usoni na kwenye koo, ugumu wa kupumua, kasi ya mapigo ya moyo, kizunguzungu, na udhaifu, Dalili hizi huanza baada ya dakika chache hadi saa chache baada ya chanjo.

Ninafaa kufanya nini?

- Ikiwa unafikiria ni mzio mkali au jambo lingine la dharura ambalo haliwezi kusubiri, piga simu kwa 9-1-1 au umpeleke mtu katika hospitali iliyo karibu nawe. La sivyo, mpigie daktari wako simu.
- Baadaye, mzio unafaa kuripotiwa kwa Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo (VAERS). Daktari wako anaweza kutoa ripoti hii, au unaweza kufanya hivyo mwenyewe kupitia tovuti ya VAERS katika **www.vaers.hhs.gov**, au kwa kupiga simu kwa **1-800-822-7967**.

VAERS huwa haitoi ushauri wa kimatibabu.

6 Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa

Programu ya Fidia ya Majeraha ya Chanjo ya Kitaifa (VICP) ni programu ya shirikisho iliyoundwa kuwafidia watu ambao huenda wakawa wamejeruhiwa na chanjo fulani.

Watu wanaoamini wamejeruhiswa na chanjo wanaweza kupata maelezo kuhusu programu hii na kuhusu kuripoti madai kwa kupiga simu kwa **1-800-338-2382** au kutembelea tovuti ya VICP katika **www.hrsa.gov/vaccinecompensation**. Kuna kikomo cha muda wa kuripoti madai ya fidia.

7 Ninaweza kupata maelezo zaidi aje?

- Muulize daktari wako. Anaweza kukupatia kipeperushi cha furushi la chanjo au kupendekeza vyanzo vingine vya maelezo.
- Piga simu kwa idara ya afya iliyo karibu na wewe au ya jimbo.
- Wasiliana na Vituo vya Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa (CDC):
  - Piga simu kwa **1-800-232-4636** (**1-800-CDC-INFO**) au
  - Tembelea tovuti ya CDC katika **www.cdc.gov/vaccines**

Vaccine Information Statement
Hib Vaccine - Kiswahili
4/02/2015
Office Use Only
42 U.S.C. § 300aa-26
Translation provided by Minnesota Department of Health

Kuwawezesha wahudumu wa afya kupata habari sahihi juu ya kinga maradhi, upimaji wa kinga maradhi, na ratiba iliyopendekezwa ya utoaji wa kinga maradhi hapo mbeleni, habari zitatumwa kwenye kituo cha Usajili wa uboreshaji huduma za Matibabu cha Michigan (Michigani Care Improvement Registry). Watu binafsi wana haki ya kuomba kwamba mhudumu wao wa afya asitume habari zinazohusu kinga maradhi kwenye kituo cha usajili.

DCH-0449SW AUTH: P. H. S., Act 42, Sect. 2126.